JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

Halmashauri ya Manispaa ya Lindi

---

**MUHTASARI WA KIKAO CHA KAWAIDA CHA BODI YA ZABUNI ROBO YA PILI KILICHOFANYIKA TAREHE 07.12.2021 KATIKA OFISI ZA KITENGO CHA MANUNUZI NA UGAVI**

MAHUDHURIO

| | |
|---|---|
| 1. Erasmo Tellun | Mwenyekiti |
| 2. Stephen Mhina | Katibu |
| 3. Omary Maje | Mjumbe |
| 4. Kihanza; B.J | Mjumbe |
| 5. Eng. Godfrey Msoma | Mjumbe |
| 6.Lazaro D. Shija | Mwanasheria |

WAJUMBE WASIOHUDHURIA

| | |
|---|---|
| Judica J. Sumari | Amehama |

**SEKRETARIETI**

| | |
|---|---|
| 1. Florence Kalimwa | PMU |
| 2.Mariam Chitanda | PMU |

**HML/BZ/MHT/2021/2022/ NA. 08: KUFUNGUA KIKAO**

Katibu alieleza kuwa kikao hicho ni cha kawaida cha robo ya pili , na kisha alimkaribisha Mwenyekiti kwa ajili ya kufungua kikao. Kabla ya kufungua kikao Mwenyekiti aliwasihi Wajumbe kutumia muda mfupi kujadili agenda zitakazowasilishwa lakini kwa umakini, kisha alifungua kikao mnamo saa 2.00 Asubuhi.

**HML/BZ/MHT/2021/2022/ NA. 09 KUPOKEA AGENDA**

Jumla ya agenda Saba (11) zilipokelewa na Wajumbe katika kikao hicho kama ifuatavyo;

1. .Kufungua kikao



Scanned with CamScanner

2. Kupokea agenda za Kikao
3. Kusoma na Kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha Tarehe 17.08.2021
4. Yatokanayo na kikao kilichopita
5. Kupokea na kuidhinisha Taarifa ya Manunuzi robo ya kwanza
6. Kupokea na kuidhinisha Taarifa ya ujenzi wa vyumba vya Madarasa kwa Shuke za Msingi na Sekondari
7. Kupokea na Kuidhinisha Taarifa ya Ujenzi wa Vituo vya Afya Mvuleni, Ng'apa na Hospitali ya Manispaa
8. Kupokea Taarifa ya Manunuzi mbalimbali yaliyoidhinishwa kupitia Waraka wa Mezani (Circular resolution)
9. Kupokea na Kuidhinisha Tangazo la uuzaji wa Mali Chakavu
10. Mengineyo kwa idhini ya Mwenyekiti
11. Kufunga Kikao

**HML/BZ/MHT/2021/2022/ NA 10 KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHUTASARI WA KIKAO KILICHOPITA CHA TAREHE 17/08/2021.**

Katibu alisoma muhutasari wa kikao kilichopita na kufanyiwa masahihisho kama ifuatavyo.

Ukurasa wa Pili HML/BZ/MUHT.Na 02 maneno **'kupokea agenda'** yaonekane, Ukurasa wa tatu HML/BZ/MUHT.Na 05 aya ya nne Mstari wa kwanza neno Kuwa lisomeke **"kua"**. Baada ya masahihisho ya Muhtasari huo Wajumbe walidhia usainiwe kwa ajili ya kumbukumbu rasmi.

**HML/BZ/MHT/2021/2022/ NA 11 YATOKANAYO NA KIKAO CHA TAREHE 17/08/2021**

Kuhusu mchakato wa ujenzi wa vyoo katika stendi ya malori sabasaba na stendi kuu ya mabasi awali ilielezwa kuwa ujenzi utafanyika kwa kuingia ubia na Mkandarasi,Lakini zoezi la kuingia ubia lilistishwa na kwamba mradi utatekelezwa na Halmashauri yenyewe kupitia mfumo wa nguvu kazi (Force account). Kuhusu taarifa ya ujenzi wa Barabara za Uhuru, Msonobari na Mchinga, ilielezwa kuwa Mtaalam Mshauri amepima kazi zilizofanyika ili kuandaa cheti cha utekelezaji. Pia ametambua kazi zote ambazo hazijatekelezwa na taarifa yake itawasilishwa katika kikao kijacho.

**HML/BZ/MHT/2021/2022/ NA 12.KUPOKEA NA KUIDHINISHA TAARIFA YA MANUNUZI ROBO YA KWANZA**

Ilielezwa na katibu kuwa Kitengo cha Manunuzi na ugavi kuanzia mwezi Julai hadi Septemba manunuzi yaliyofanyika yalikuwa jumla ya tzs; 136,936,913.31. Bodi ya Zabuni ilipokea taarifa hiyo.

**HML/BZ/MHT/2021/2022/ NA 13: KUPOKEA NA KUIDHINISHA TAARIFA YA UJENZI WA VYUMBA VYA MADARASA KWA SHUKE ZA MSINGI NA SEKONDARI**

Ilielezwa kuwa idara ya Elimu Msingi ilipokea kiasi cha **Tshs; 420,000,00** kwa ajili ya ujenzi wa vyumba ishirini na moja (21) vya Madarasa na Shule Shikizi nane ( 8) Kupitia Program ya Covid 19, Vilevile kiasi cha Tshs; 160,000,000 zilipokelewa kutoka Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya Madarasa Sita (6) na Matundu ya vyoo ishirini na nne 24). Aidha katibu aliendelea kueleza kuwa Vile vile fedha nyingine zilizopokelewa kwa ajili ya ujenzi



Scanned with CamScanner

...aliziaji wa vyumba vya madarasa (8) ni Tshs;225,000,000. Fedha hizi ni Ruzuku ya Miradi ...Maendeleo.

Katibu aliendelea kutoa Maelezo kuwa Fedha zilizotolewa na program ya covid shule zilizonufaika na Mradi huo ni

1. Cheleweni shule ya msingi Madarasa mawili (2) kiasi cha Tsh; 40,000,000.00
2. Mnazimmoja Shule ya Msingi Madarasa Mawili (2)kiasi cha Tshs; 40,000,000.00
3. Tulieni Shule ya Msingi Madarasa mawili (2) kiasi chaTshs; 40,000,000.00
4. Kitumbikwela Shule ya Msingi Marasa mawili Kiasi cha Tshs 40,000,000.00
5. Kilangala Shule ya Msingi Madarasa mawili( 2) kiasi cha Tshs 40,000,000.00
6. Kitomanga Shule ya Msingi Madarasa Manne (4) Kiasi cha Tshs 80,000,000.00
7. Kikwetu Shule ya Msingi Madarasa Manne (4) Kiasi cha Tshs 80,000,000.00
8. Nangaru Shule ya Msingi Madarasa matatu (3) Kiasi Cha Tshs 60,000,000.00

VileVile ilielezwa kuwa katika ujenzi na umaliziaji wa shule nane (8) kupitia fedha za ruzuku ya Miradi ya Maendeleo Shule zilizopatiwa fedha ni kama ifuatavyo;

1. Ruchemi Shule ya Msingi madarasa Mawili (2) Kiasi cha Tsh ; 40,000,000.00
2. ,Mnyangara Shule ya Msingi Madarasa Mawili (2) Kiasi cha Tshs; 25,000,000.00
3. Makumba Shule ya Msingi Madaras Mawili (2) Kiasi cha Tshs; 25,000,000.00
4. Mtumbikile Shule ya Msingi Madarasa Mawili (2) Kiasi Cha Tshs 20,000,000.00
5. Mkwaya Shule ya Msingi Madarasa Mawili (2) Kiasi Cha Tshs; 40,000,000.00
6. Ruaha Shule ya Msingi Madarasa Mawili (2) Kiasa Cha Tshs 25,000,000.00
7. Tulien Shule ya Msingi Madarasa Mawili (2) Kiasi Cha Tshs 25,000,000.00
8. Chikonji Kaskazini Shule ya Msingi Mawili (2) Kiasi cha Tshs; 25,000,000.00

**HML/BZ/MHT/2021/2022/ NA 14: KUPOKEA NA KUIDHINISHA TAARIFA YA UJENZI WA VITUO VYA AFYA MVULENI, NG'APA NA HOSPITALI YA MANISPAA**

Katibu Alieleza kupitia taarifa iliyowasilishwa kuwa, Idara ya Afya Imepokea fedha za ujenzi Kiasi cha Tzs; 600,000,000.00 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya na umaliziaji wa Zahanati Mbili ambazo ni Zahanati ya Ruaha na Zahanati ya Nanyanje,Sambamba na Taarifa hiyo Ilielezwa kuwa Idara ya Afya kwa kipindi hicho hicho kuna fedha zilipokelewa kiasi cha Tzs;500,000,000.00 ikiwa ni kwa ajili ya ujezi wa Vituo Viwili ambavyo ni Kituo cha Afya Mvulen na Kituo cha Afya Ng'apa Wajumbe Kwa pamoja walipokea Taarifa hiyo na kuwa miradi iendelee kutekelezwa kupitia mfumo wa nguvu kazi (Force Account). Aidha Bodi ya Zabuni iliagiza nyaraka muhimu kwa ajili ya miradi inayotekelezwa kupitia mfumo huu ziwe zinawasilishwa kama taratibu zinavyohitaji. Katibu alieleza kuwa nyaraka muhimu zinazopaswa kuwasilishwa Bodi ya Zabuni katika hatua ya utoaji wa idhini ni Tangazo la kumpata fundi pamoja na Ankra kifani (BOQ).

**HML/BZ/MHT/2021/2022/ NA 15: .KUPOKEA TAARIFA YA MANUNUZI MBALIMBALI**

Taarifa hiyo iliwasilishwa katika kikao hicho ikielezea kuwa, kwa kipindi cha robo ya pili kitengo cha Manunuzi na ugavi kimefanya manunuzi mbalimbali kupitia waraka wa Maoni (circular Resolution ) yenye Jumla ya Shilingi 47,779,234.08 hii ni kwa mujibu wa sheria ya Manunuzi kwamba Manunuzi yanayofanyika kwa njia ya waraka yanaripotiwa katika kikao cha bodi ya zabuni.Manunuzi hayo ni Ununuzi wa taili za mtambo wenye namba za usajili SM 12032 kwa gharama ya Tzs; 5,350,000.00 kampuni ya BS Tyre Centre,Ununuzi wa mafuta kwa ajili ya shughuri za mitihan Tzs;12,611,500.00 Mzabuni Najima petrol Station,Ununuzi wa vifaa vya Ukarabati wa nyumba ya Mkurugenzi Tsz; 4,450,000.00 Mzabuni Sayona Traders,Matengenezo ya



Scanned with CamScanner

Gari Tzs;11,528,600,00 yenye namba za usajil SM 11773 Kampuni ya Kahawa Motors Tanzanian LTD.,Matengenezo ya gari Tzs; 5,814.634.08 gari yenye usajili wa Namba SM11784 kampuni ya GF Truck Equipment LTD ,ununuzi wa Mtambo wa Kufyatulia Tofali kwa gharama ya Tzs;8,024,000.00 kamupuni y Mtanga Pollymachinery. Pia iliwasilishwa taarifa ya Manunuzi mbalimbali yaliyofanyika kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2021/2022 ambayo ni kiasi cha Tshs. 67,494,537.31.

Pamoja na taarifa hii Katibu aliwataarifu Wajumbe wa Bodi ya Zabuni kuwa, yapo Manunuzi ambayo hayajawasilishwa katika vikao vya Bodi vilivyopita yenye thamani ya Tshs. 144,618,617.00. Manunuzi haya yalifanyika kwa njia ya masurufu kwa hiyo imekuwa vigumu kwa Kitengo cha Ununuzi na Ugavi kupata taarifa zake kwa wakati.

Baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hiyo ilipokelewa na wajumbe.

**HML/BZ/MHT/2021/2022/ NA 16: KUPOKEA NA KUIDHINISHA TANGAZO LA UUZAJI WA MALI CHAKAVU**

Ilielezwa na katibu wa Bodi ya Zabuni kuwa kwa kipindi kirefu kumekuwa na ufuatiliaji wa kibali cha kuondosha mali chakavu kutoka kwa Katibu Mkuu Wizara ya fedha na uchumi.Alieleza kuwa kufikia tarehe ya kikao hicho, kibali kimetolewa kuwa mali zitauzwa kwa njia ya Mnada. Mjumbe mmoja alitaka kujua endapo Watumishi wa Manispaa wanapewa kipaumbele gani katika zoezi hili ili kununua baadhi ya mali. Ilelezwa kuwa, kibali kilichotolewa kinaitaka Halmashauri kuuza mali zilizopo kwa njia ya mnada bila kutoa upendeleo wowote maalum kwa Watumishi wake.

Baada ya Maelezo hayo wajumbe waliidhinisha tangazo la uuzaji wa Mali chakavu kwa njia ya mnada.

**HML/BZ/MHT/2021/2022/ NA 17: MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI**

Hapakuwa na mengineyo katika kikao hiki.

**HML/BZ/MHT/2021/2022/ NA 18: KUFUNGA KIKAO**

Katibu alimkaribisha Mwenyekiti ili afunge kikao.Mwenyekiti alianza kwa kuwashukuru wajumbe kwa uvumilivu wao pamoja na michango yao yenye tija .Baadaya ya kusema hayo alifunga kikao mnamo saa 5;30 Asubuhi

| | |
|---|---|
| ............................... | ............................... |
| Steven R. Mhina | Erasimo Tellun |
| Katibu | Mwenyekiti |

Tarehe 25/04/2022.



Scanned with CamScanner